ama viongozi ambao wakati wa shida watatukimbia au kusubiria kupata maelekezo kutoka kwa wale wanaowatuma.

"Uamuzi ni wenu, lakini ninawaomba ndugu zangu wana Dodoma na Watanzania kwa ujumla mlitafakari hili kwa ajili ya masilahi mapana ya taifa letu na hii ndio sababu nasema uchaguzi huu ni muhimu sana ambao kila Mtanzania hana budi kushiriki na kufanya maamuzi yaliyosahihi kwa maendeleo, ustawi na mustakabali mzima wa taifa letu," alisema Dkt. Magufuli.

Dkt. Magufuli alisema chama pekee chenye uwezo wa kuwaletea maendeleo ya kweli Watanzania na kudumisha amani, umoja na mshikamano wan chi yetu ni Chama Cha Mapinduzi.

"Hivyo ndugu zangu Watanzania ninaomba sana kura zenu tupate kura zote mkipigie Chama Cha Mapinduzi kura za Rais, kura za wabunge, kura za wawakilishi, kura za madiwani na utakapofika uchaguzi kule Zanzibar kura za Rais wa Zanzibar ili haya niliyoyaeleza hapa tuweze kuyatekeleza kwa kasi zaidi" alisema Dkt. Magufuli.

Dkt. Magufuli alisema katika

"Ninawaomba siku ya kupiga kura msije mkasema Magufuli ameshinda au wabunge wa

riba katika mabenki yetu.

Pia miaka mitano ijayo pia

Dkt. Magufuli alisema kwa upande wa mifugo

nyingine tupeni tukayatekeleze," alisema Dkt. Magufuli.

# Agizo la Mpina ng'ombe walioibwa latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu, Siha**

AGIZO lililotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina kuhusiana na kashfa ya wizi wa ng'ombe 17 wenye thamani ya sh.milioni 14 katika Ranchi ya Taifa ya West Kilimanjaro limetekelezwa baada ya Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu kukabidhiwa ng'ombe hao baada waliokuwa watumishi wa ranchi hiyo kununua wengine.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema ng'ombe amekabidhiwa na Meneja wa Kampuni hiyo, Mbelwa Lutagwelera ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mpina aliyeagiza ngombe kurejeshwa kwenye ranchi na kukataa sababu zilizokuwa zimetolewa kuwa ng'ombe wameibiwa.

"Ni kweli nimepokea leo ng'ombe hao baada ya kurejeshwa kama Waziri alivyoagiza alipotembelea Ranchi hii kwamba mifugo hiyo ipatikane haraka na hatua ziendelee kuchukuliwa kwa wote waliohusika na kashfa hiyo," alisema Buswelu.

Pia Mkuu huyo wa wilaya ameagiza Menejimenti ya NARCO kuajiri walinzi wenye sifa na hasa waliopitia mafunzo kutoka kutoka Jeshi la Akiba ambao wamefundishwa uadilifu na uzalendo wa nchi yao, badala ya kuajiri watu wasiokuwa na sifa.

Buswelu aliwataka watumishi wa ranchi hiyo kusimamia ulinzi wa rasilimali za kampuni hiyo na kujiepusha na vitendo vya kuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi na badala yake wazalishe ng'ombe wengi ili taifa lipate fedha nyingi kutokana na mifugo.

Wakati Waziri Mpina alipotembelea Ranchi hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo aliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata kwa watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro kufuatia kashfa ya kupotea kwenye Mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa Serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buselu alisema tangu wizi huo ufanywe hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo jambo linaonesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiibia Serikali jambo ambalo halikubaliki.

Hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvivi, Luhaga Mpina alipoitembelea wilaya hiyo, alieleza kutokuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa Ranchi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza kuwa ifikapo jumatano Julai 19 mwaka huu mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya Ranchi hiyo.

Waziri Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Akitoa taarifa kuhusu kampuni hiyo, Kaimu Meneja wa NARCO, Lutagwelera alisema kwa sasa wataendelea kushirikiana na Serikali ya wilaya hiyo katika kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo ili vitendo kama hivyo visitokee tena ili kuongeza uzalishaji mifugo kwenye ranchi hiyo.

Scanned with CamScanner

Treni ya mizigo ikiwasili katika Stesheni ya Krokon jijini Arusha, ikiwa na Shehena ya Saruji Tani 320 kutoka Kampuni ya Tanga Cement ya jijini Tanga, hivi karibuni. Treni hiyo iliyokuwa na mabehewa nane ilipokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, ikiwa sehemu ya safari ya majaribio kutoka Tanga kwenda Arusha. **NA MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 4.

# Wafugaji wadaiwa kuua mgambo, 8 wajeruhiwa

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

ASKARI wa Jeshi la akiba (mgambo) katika Kijiji cha Machema Kata ya Nampungu, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Said Katimbe (46), ameuawa kwa kuchomwa mkuki kifuani na wanaodaiwa kuwa ni watu wa jamii ya kifugaji.

Katimbe anadaiwa kuchomwa mkuki mara mbili katika mapigano kati ya wafugaji na wakulima.

Aidha, katika tukio hilo watu wanane walijeruhiwa na wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, baada ya kujeruhiwa na silaha za jadi zinazodaiwa kutumiwa na wafugaji.

Mtendaji wa Kijiji cha Machemba, Ally Sapanga, aliwataja waliojeruhiwa ni Zuberi Jafari, Mohammed Chikoko, Mohammed Lilundu, Jimu Mbandawe, Issa Saidi, Matumula Selemani, Zuberi Nasoro na Mohammed Sengani.

Alisema mapigano hayo yalizuka Agosti 28, mwaka huu, majira ya saa 11.30 jioni baada ya wafugaji hao kuvamia kijiji humo na kuwashushia kipigo watu waliokuwa katika sherehe za harusi bila kuuliza wa kupewa nafasi ya kujitetea.

Mtendaji huyo alibainisha kuwa kuna taarifa zinaeleza kuwa chanzo cha mapigano hayo ni wafugaji hao kuhisi kuwa wakazi wa Kijiji hicho kuiba mifugo yao iliyodaiwa kuwa ilipotea kwa kutoweka kwenye kambi zao.

Sepanga alisema wafugaji waliowashambulia kwa kutumia fimbo, sime, mikuki na mishale hali iliyosababisha taharuki na kuwafanya wananchi kukimbia kwa lengo la kujiokoa.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa alituma askari kutoka katika kituo cha polisi Tunduru kufuatilia na kuwatafuta wafugaji wanaodaiwa kufanya kitendo hicho.

Alisema kitendo cha wafugaji kuchukua sheria mikononi kimewaondolea haki yao kisheria hata kama walikuwa na hoja au madai ya msingi katika tukio hilo.

Aidha, Kamanda Maigwa aliwataka wananchi wenye taarifa za maeneo waliyokimbilia watuhumiwa hao kwa lengo la kujificha, kutoa taarifa Polisi ili wakamatwe na kupisha sheria kufuata mkondo wake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuwahamishia wafugaji hao katika maeneo ya vitalu vilivyotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Walidai kuwa wafugaji badala ya kuishi kwenye vitalu hivyo, wamevamia na kulisha mifugo yao kwenye makazi ya watu.

## ...kashfa wizi wa ng'ombe 17 latekelezwa

**TULINDE MAZINGIRA: Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Chistopher Ngubiagai akimwagilia mti alioupanda kwenye chanzo cha maji cha mto Mavuji, wakati wa uzinduzi wa uhifadhi wa chanzo hicho wilayani Kilwa juzi.**

MTANZANIA UK5.

# Ng'ombe 17 wa Serikali waliopotea warejeshwa

**Na MWANDISHI WETU - SIHA**

AGIZO lililotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina kuhusu kashfa ya wizi wa ng'ombe 17 wenye thamani ya Sh milioni 14 katika Ranchi ya Taifa ya West Kilimanjaro, limetekelezwa baada ya Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu kukabidhiwa ng'ombe hao waliokuwa watumishi wa ranchi hiyo kununua wengine.

Akizungumza mjini hapa jana, Buswelu, alisema amekabidhiwa ng'ombe na Meneja wa Kampuni hiyo, Mbelwa Lutagwelera ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mpina aliyeagiza kurejeshwa kwenye ranchi na kukataa sababu zilizokuwa zimetolewa kuwa wameibiwa.

"Nimepokea ng'ombe hawa,baada ya kurejeshwa kama waziri alivyoagiza alipotembelea ranchi hii,mifugo hii ipatikane haraka na hatua ziendelee kuchukuliwa kwa wote waliohusika na kashfa hiyo"alisema Buswelu.

Aliagiza menejimenti ya NARCO kuajiri walinzi wenye sifa na hasa waliopitia mafunzo kutoka kutoka jeshi la akiba ambao wamefundishwa uadilifu na uzalendo wa nchi yao, badala ya kuajiri watu wasiokuwa na sifa.

Aliwataka watumishi wa ranchi kusimamia ulinzi wa rasilimali za kampuni na kujiepusha na vitendo vya kuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi na badala yake wazalishe ng'ombe wengi ili taifa lipate fedha nyingi kutokana na mifugo.

Mkuu wa wilaya aliagiza polisi kuwakamata watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro kutokana na kashfa ya kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa Serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buselu alisema tangu wizi huo ufanywe hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, jambo linaonesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiibia Serikali jambo ambalo halikubaliki.

Alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Kaimu Meneja wa NARCO, Lutagwelera alisema kwa sasa wataendelea kushirikiana na Serikali ya wilaya hiyo katika kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo ili vitendo kama visitokee tena ili kuongeza uzalishaji mifugo kwenye ranchi hiyo.

# Wanufaika waomba kuendelea kusaidiwa

Scanned with CamScanner

cha Guavay, Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), Dk Stephano Ngailo na kushoto ni Meneja Ubora wa kiwanda hicho, Latifa Mafumbi. Kiwanda hicho cha vijana watanzania kina uwezo wa kuzalisha tani 2,000 za mbolea kwa mwaka. (Picha na Wizara ya Kilimo).

HABARI LEO UK 17.

# Wajasiriamali wafunzwa kufuga kuku

**Na Veronica Mheta, Arusha**

WAJASIRIAMALI wa Jiji la Arusha wamemshukuru Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi kwa kuwawezesha kupata mafunzo yakiwemo ya ufugaji kuku, utengezaji batiki na kuunganishwa na fursa za mikopo katika benki za NMB na CRDB.

Wamesema ni nadra kwa kiongozi kama huyo, kutoa elimu bure kwa wajasiriamali kuhusu ututoleshaji vifaranga, utengezaji batiki, utengezaji sabuni za unga na maji, kupanda vitunguu na kutengeneza pilipili.

Walisema elimu waliyopata wataitumia vema kujikwamua kiuchumi na kupata mikopo katika benki hizo, kwa kuwa bidhaa watakazozalisha zitakubalika .

"Tunashukuru DC Kihongosi kwa sababu si mchoyo wa fursa za kimaendeleo, tumejifunza jinsi ya kutotolesha vifaranga wengi kwa njia za boksi la kawaida, utengezaji wa sabuni na mengi "alisema mjasirimali Lilian Joseph.

Mjasiriamali mwingine, Issa Mohamed alisema utengezaji batiki ni mojawapo ya fursa zilizopo sokoni. Alisema kwamba watatengeneza vikoi vya aina mbalimbali kwa sababu Jiji la Arusha ni la utalii, hivyo kuwezeshwa kwa mafunzo hayo kutawawezesha kutoka kwenye umasikini.

Kihongosi alisema ameamua kutoa mafunzo hayo kwa siku mbili, kuwezesha wajasiriamali kujikwamua kiuchumi. Alisema amepigwa vita na watu, wakidai kazi ya ukuu wa wilaya ni kuwatumia wananchi na si kutoa mafunzo kwa wajasiriamali.

Alisema ameamua kutoa elimu hiyo kwa wajasiriamali wajikwamue kiuchumi, kwa kwa yeye awali alipomaliza chuo hakupata ajira serikalini, bali aliajiri katika ujasiriamali ukiwemo kufuga nyuki.

"Nimeamua kutumia elimu yangu kuwasaidia wajasiriamali hawa sambamba na kuwaunganisha na masoko ikiwemo fursa za kibiashara kwa kukopa benki hizo mbili ili wajikwamue kiuchumi"alisema Kihongosi.

Nyamugari, Kibande, Migongo, Muyamana Kilelema.

kujeruhiwa na silaha za jadi zinazodaiwa kutumiwa na wafu-

hayo ni wafugaji hao kuhisi kuwa wakazi wa Kijiji hicho kui-

kufanya kitendo hicho.

Alisema kitendo cha wafugaji kuchukua sheria mikononi

ya kuishi kwenye vitalu hivyo, wamevamia na kulisha mifugo yao kwenye makazi ya watu.

# Agizo la Mpina kashfa wizi wa ng'ombe 17 latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

AGIZO lililotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuhusiana na kashfa ya wizi wa ng'ombe 17 wenye thamani ya Sh. milioni 14 katika Ranchi ya Taifa ya West Kilimanjaro limetekelezwa.

Utekelezaji huo umefanyika baada ya Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, kukabidhiwa ng'ombe hao baada waliokuwa watumishi wa ranchi hiyo kununua wengine.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema ng'ombe amekabidhiwa na Meneja wa Kampuni hiyo, Mbelwa Lutagwelera, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mpina aliyeagiza ngombe kurejeshwa kwenye ranchi na kukataa sababu zilizokuwa zimetolewa kuwa ng'ombe wameibiwa.

"Ni kweli nimepokea leo ng'ombe hao baada ya kurejeshwa kama Mh. Waziri alivyoagiza alipotembelea Ranchi hii kwamba mifugo hiyo ipatikane haraka na hatua ziendelee kuchukuliwa kwa wote waliohusika na kashfa hiyo," alisema Buswelu.

Pia Mkuu huyo wa wilaya ameagiza Menejimenti ya NARCO kuajiri walinzi wenye sifa na hasa waliopitia mafunzo kutoka kutoka Jeshi la Akiba ambao wamefundishwa uadilifu na uzalendo wa nchi yao, badala ya kuajiri watu wasiokuwa na sifa.

Buswelu aliwataka watumishi wa ranchi hiyo kusimamia ulinzi wa rasilimali za kampuni hiyo na kujiepusha na vitendo vya kuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi na badala yake wazalishe ng'ombe wengi ili taifa lipate fedha nyingi kutokana na mifugo.

Wakati Waziri Mpina alipotembelea Ranchi hiyo, Mkuu wa wilaya hiyo aliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata kwa watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro kufuatia kashfa ya kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa Serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buselu amesema tangu wizi huo ufanywe hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo jambo linaoonesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiibia Serikali jambo ambalo halikubaliki.

Hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alipoitembelea wilaya hiyo, alieleza kutokuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa Ranchi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza kuwa ifikapo jumatano Julai 19, mwaka huu mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya Ranchi hiyo.

Waziri Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Akitoa taarifa kuhusu kampuni hiyo, Kaimu Meneja wa NARCO, Lutagwelera alisema kwa sasa wataendelea kushirikiana na Serikali ya wilaya hiyo katika kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo ili vitendo kama hivyo visitokee tena ili kuongeza uzalishaji mifugo kwenye ranchi hiyo.

Scanned with CamScanner

UHURU UK 18.

# Neema mpya ya ajira machinjio ya Vingunguti yaja

**Na SIMON NYALOBI**

UONGOZI wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Vingunguti, Wilaya ya Ilala, Jijini Dar es Salaam, umesema umefarijika kwa ujio wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti, kwa kuwa yatatoa ajira nyingi kwa vijana wa kata hiyo.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Katibu wa Elimu na Malezi wa jumuiya hiyo, Halima Pombe, alipozungumza na Uhuru, baada ya kufanyika kwa mkutano wa baraza la wazazi wa kata hiyo.

Halima, alisema wajumbe wa baraza hilo kwa kauli moja waliunga mkono ujio wa machinjio hiyo, inayojengwa na serikali kwa kuwa itakuwa sehemu ya kupunguza tatizo la ajira, hususan vijana wa kata hiyo.

"Sisi kama wajumbe wa baraza la wazazi, tulizungumza na aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto, akatueleza pale kutakukuwa na ajira 200 zisizo za kitaaluma na nyingine ambazo zitakuwa za kitaaluma.

"Kwa hiyo tuna uhakika wa vijana wetu kupata ajira, na hiyo itapunguza idadi ya vijana wasio na ajira, ikizingatiwa kuwa tatizo hilo limekuwa likilalamikiwa na baadhi yao,"alisema.

Akizungumzia ujenzi wa barabara za ndani katika kata hiyo, alisema jumuiya hiyo imefarijika kwa majibu ya serikali kuwa, zipo katika mpango wa ujenzi chini ya Mradi wa Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Alisema baada ya mradi huo kukamilika, barabara za mitaa hiyo zitakuwa katika muonekano bora na kupendezesha kata hiyo.

Alisema kwa sasa, kilio kikubwa kwa wakazi hao ni barabara hizo, hivyo kuwataka wawe na uvumilivu wakati wakisubiri ujio wa mradi huo.

Kwa upande wake, Katibu wa Wazazi wa kata hiyo, Sharifa Sinde, alisema jumuiya hiyo imejipanga vizuri kukisaidia Chama kushika dola.

Sharifa, alisema wamewaandaa makatibu wa matawi wakishirikiana na jumuiya nyingine za Chama, ambazo ni Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Umoja wa Vijana (UVCCM), kuhakikisha ushindi mkubwa unapatikana katika uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu.

**Ajira**

**VIJANA WASIO NA KAZI WATAPUNGUA**

Kwa hiyo tuna uhakika wa vijana wetu kupata ajira, na hiyo itapunguza idadi ya vijana wasio na ajira, ikizingatiwa kuwa tatizo hilo limekuwa likilalamikiwa na baadhi yao.

Scanned with CamScanner